

102/3
KISWAHILI
Karatasi 3
FASIHI
Okt./Nov. 2008
Saa 2½

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
Kenya Certificate of Secondary Education
KISWAHILI
Karatasi 3
FASIHI
Saa 2½

Maagizo

Jibu maswali manne pekee.

Swali la kwanza ni la lazima.

Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani:

Tamthilia, Riwaya, Hadithi Fupi na Fasihi simulizi.

Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.

Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii
zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

1 (LAZIMA)

USHAIRI

Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

WASAKATONGE1. **Wasakatonge na juakali**

Wabeba zege ya maroshani,
Ni msukuma mikokoteni,
Pia makuli bandarini,
Ni wachimbaji wa migodini,
Lakini maisha yao chini.

2. **Juakali na wasakatonge**

Wao ni manamba mashambani,
Ni wachapa kazi viwandani,
Mayaya na madobi wa nyumbani,
Ni matopasi wa majaani,
Lakini bado ni masikini.

3. **Wasakatonge na juakali**

Wao huweka serikalini,
Wanasiasa madarakani,
Dola ikawa mikononi,
Wachaguliwa na ikuluni,
Lakini wachaguaji duni.

4. **Juakali na wasakatonge**

Wao ni wengi ulimwenguni,
Tabaka lisilo ahueni,
Siku zote wako matesoni,
Ziada ya pato hawaoni,
Lakini watakomboka lini?
(Mohammed Seif Khatib)

- (a) “Shairi hili ni la kukatisha tamaa”. Fafanua rai hii kwa kutoa mifano minne. (alama 4)
- (b) Taja tamathali ya usemi iliyotawala katika shairi zima na uonyeshe mifano miwili ya jinsi ilivyotumika. (alama 3)
- (c) Eleza umbo la shairi hili. (alama 5)
- (d) Andika ubeti wa tatu katika lugha ya nathari. (alama 4)
- (e) Onyesha mifano miwili ya maadili yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 2)

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi.

- (i) Manamba
(ii) Tabaka lisilo ahueni (alama 2)

TAMTHILIA

Jibu swali la 2 au la 3.

Kithaka wa Mberia: *Kifo Kisimani*

- 2 Ukitumia mifano, onyesha matumizi matano ya mbinu ya ishara kama ilivyotumiwa katika tamthilia ya *Kifo Kisimani*. (alama 20)
- 3 “Kwa hakika, kama mzazi hana kifani katika Butangi nzima. Na pengine hata katika ulimwengu mzima.”
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (b) “Watu waliojiita washauri wa Mtemi Bokono walikuwa si washauri halisi bali wanafiki waliomdanganya.” Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano mitano. (alama 16)

RIWAYA

Jibu swali la 4 au la 5.

Z. Burhani: *Mwisho wa Kosa.*

- 4 “Wanawake katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* wamepewa nafasi ndogo katika masuala ya maendeleo ya kijamii.” Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano kumi. (alama 20)
- 5 Eleza jinsi wahusika wafuatao wanavyoafiki anwani ya riwaya ya *Mwisho wa Kosa*:
- (a) Ali (alama 10)
- (b) Asha (alama 10)

HADITHI FUPI

K. W. Wamitila (*mhariri*): *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*

- 6 “Umdhaniaye ndiye, kumbe siye”.
Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*, onyesha ukweli wa kauli hii. (alama 20)

FASIHI SIMULIZI

- 7 Fafanua sifa zozote kumi za mtambaji bora wa ngano. (20 alama)